# Maktaba za Umma za Ushirika wa Kaunti ya Lancaster
# Sera ya Matumizi Yanayokubalika ya Intaneti na Kompyuta

*Maktaba za umma za Kaunti ya Lancaster zinafanya jitihada ya kukidhi mahitaji ya kitamaduni, habari na kielimu ya jumuiya tunazohudumia.*

Mfumo wa Maktaba wa Kaunti ya Lancaster (LSLC) ni muungano wa maktaba zinazoundwa na maktaba binafsi za umma katika Kaunti ya Lancaster, matawi yao, maktaba inayotembea na ofisi za utawala. Sera hii inahudumia vitengo, wafanyakazi na wajitoleaji wote wa LSLC na huduma zote zinazotolewa mahali ulipo na kwa masafa. Sera hii inashughulikia kwa usawa maeneo halisi na wawakilishi wa kibinadamu wa LSLC.

## Shabaha ya Sera:

LSLC (LSLC, maktaba husika, maktaba au maktaba za umma) itatoa ufikio sawa wa rasilimali za kielektroniki kwa watu binafsi (mtumiaji, watumiaji). Maktaba inaweza kurekebisha sera hii kwa nyongeza zinazoendana na hali na jumuiya yao.

## Ufikio wa Intaneti:

Ufikio sawa wa rasilimali za intaneti ni chaguo muhimu. Intaneti ni njia isiyodhibitiwa na si taarifa zote zinafaa kwa hadhira zote. Baadhi ya taarifa si sahihi, zinakera, na/au haramu. Ingawa maktaba zinatumia programu ya kuchuja kwa mujibu wa Sheria ya Usalama wa Intaneti kwa Watoto (CIPA), haiwezekani kuchuja/kuzuia nyenzo zote zisizofaa, zinazokukera au zisizo halali.

## Wajibu wa Wafanyakazi na Watumiaji wa Maktaba:

Ni wajibu wa mtu anayetumia rasilimali za kielektroniki kufuatilia matumizi yake binafsi na/au matumizi ya mtoto anayemtegemea. Watumiaji wanawajibika kushughulikia rasilimali na vifaa vya kielektroniki kistaarabu. Watumiaji wanapaswa kuhifadhi data kwenye kifaa cha kando au kuhifadhi taarifa zao kwa njia inayofaa kwao binafsi. Kompyuta za maktaba hazitahifadhi data ndani yake na maktaba haitawajibika kwa data iliyopotea kutokana na hitilafu ya kuhifadhi faili, kumalizika muda wa kompyuta, au sababu nyingine yoyote.

**WAZAZI WANAHIMIZWA, NA HUENDA WAKAHITAJIKA, KUJA KWENYE MAKTABA NA WATOTO WADOGO ILI KUWAANGALIA**
**RATIBA ZA INTANETI.**

## Kanusho:

- Wafanyakazi wa maktaba wanaweza kufuatilia matumizi ya mtu binafsi ya WiFi na kompyuta za umma.

- Mtumiaji, na/au mzazi/mlezi wa mtumiaji, anawajibika kwa ratiba yake ya Intaneti kila wakati.
- LSLC inakanusha dhamana yoyote kuhusu usahihi, muda wa taarifa iliyochukuliwa, mamlaka au ufaaji wake kwa kusudi mahsusi.
- LSLC, mashirika ya maktaba za umma na wafanyakazi wake hawatawajibika kwa uharibifu wa moja kwa moja, usio wa moja kwa moja au wa matokeo unaohusiana na matumizi ya rasilimali zake za kompyuta. Hii inajumuisha na haikomei kwa uharibifu wa mali, hasara ya kifedha, wizi wa utambulisho, au uharibifu wa sifa kutokana na kutumia mtandao au kompyuta za maktaba.
- Programu za kompyuta na taarifa kutoka chanzo chochote, ikiwemo Intaneti, zinaweza kuhitilafiana na kompyuta za watumiaji au vifaa vingine binafsi vya kielektroniki. Maktaba haziwajibiki kwa uharibifu wa kompyuta za watumiaji au kifaa kingine chochote cha kielektroniki au kwa upotevu wa data unaoweza kutokea kutokana na kutumia rasilimali ya maktaba au Intaneti.
- Watumiaji wanawajibika kwa uharibifu wowote wa vifaa vinavyomilikiwa na maktaba, programu za kompyuta au mtandao unaotokea wakati wa kutumia rasilimali.
- Kompyuta za maktaba hazitahifadhi mafaili na zitamwondoa mtumiaji baada ya muda mfupi wa kutofanya chochote. Maktaba haiwajibiki kwa data yoyote itakayopotea.
- Taarifa zinazosambazwa kwenye Intaneti, bila kujali ulinzi wa usalama unaotumiwa, zinaweza kuwa za umma. Watumiaji wa kompyuta wanawajibika kulinda taarifa zao binafsi. Maktaba haitawajibika kwa ukiukaji wowote wa usalama kutokana na matumizi ya kompyuta au mitandao inayomilikiwa na maktaba.

## MATUMIZI YASIYOKUBALIKA YA KOMPYUTA NA MTANDAO

Matumizi yasiyokubalika ya kompyuta na mtandao yanajumuisha na hayakomei kwa:

- Matumizi yanayokiuka sheria au kuwahimiza wengine kukiuka sheria
- Matumizi yanayosababisha madhara kwa wengine au uharibifu wa mali yao
- Matumizi yanayokiuka sera na makubaliano mengine ya maktaba.
- Matumizi yanayohatarisha usalama wa mtandao wa kompyuta au kompyuta nyingine katika Intaneti
- Matumizi yanayoonekana kuwa ya kudhuru au kuhatarisha usalama na ulinzi wa watoto. Neno "hatari kwa watoto" limefafanuliwa na Sheria ya Mawasiliano ya mwaka 1934 (47 USC Ibara ya 254 [h][7])
- Kuonesha, kupakua, au kunakili ujumbe wa kukera au usiofaa, picha au nyenzo za ngono kama ilivyofafanuliwa katika 18 Pa.CSA § 5903.
- Kukiuka sheria ya Hakimiliki ya Marekani. Sheria inakataza matumizi yasiyoidhinishwa ya nyenzo zenye hakimiliki isipokuwa imeruhusiwa na kanuni za "matumizi ya haki". Usinakili au kusambaza nyenzo za kielektroniki (ikiwemo maandishi, picha, sauti, programu, barua pepe au data) bila idhini dhahiri ya mwenye hakimiliki.
- Matumizi yanayokiuka usiri wa taarifa au kuweka utambulisho wa mtu yeyote hatarini.
- Kwa sababu za usalama, watoto wanapaswa kutotoa nywila; kutowapa wengine taarifa binafsi zao wenyewe au wengine, ikiwemo kadi ya benki na nambari za kadi ya SSN; na/au kupanga kukutana ana kwa ana na mtu aliyekutana naye kupitia Intaneti au mtandao wa kompyuta.

## TARATIBU ZA MATUMIZI YA KOMPYUTA ZA UMMA ZINAZOMILIKIWA NA MAKTABA

Ili kutumia intaneti katika kompyuta ya umma inayomilikiwa na maktaba au kifaa cha kielektroniki lazima kuwa na kadi halali ya maktaba ya LSLC. Maktaba Wanachama zinaweza kuamua kutofuata kanuni hii au kutoa ruhusa kwa mgeni kwa masharti machache ikiwa kompyuta zinapatikana.

- Lazima kusaini "Makubaliano ya Kutumia Intaneti". Akiwa chini ya miaka 18, "Fomu ya Ruhusa ya Wazazi" lazima isainiwe na mzazi au mlezi halali wa mtumiaji mbele ya mfanyakazi wa maktaba.
- Watumiaji wa kompyuta lazima waweze kutumia kompyuta kwa kujitegemea, na wanaweza kutakiwa kuonesha uwezo wao wa kutumia kompyuta bila kuiharibu.
- Watumiaji lazima waondoke kwenye kompyuta mara moja wanapoambiwa na mfanyakazi.
- Watumiaji hawapaswi kusakinisha programu kwenye kompyuta za umma au kujaribu kuongeza, kuboresha au kuondoa maunzi au programu ya kompyuta ya umma.
- Watumiaji wanaweza kupakua tu taarifa ambayo ni halali kunakili.
- Watumiaji wataepuka kutumia sauti au picha ambazo zinaweza kuwasumbua wengine.
- Maktaba Wanachama hazitoi akaunti za barua pepe. Watumiaji wanaweza kutumia kompyuta za maktaba kufikia barua pepe za watoa huduma wa nje kama vile Outlook, Yahoo, Gmail, n.k.
- Watumiaji hawapaswi kubadilisha au kuambatisha kifaa, isipokuwa flashi au hedifoni, kwenye maunzi ya maktaba, au kubadilisha, kuongeza au kujaribu kubadilisha programu au mipangilio ya kifaa. Maktaba ina haki ya kuamua kutofuata kanuni za ufikio au masuala binafsi.
- Watumiaji wanawajibika kwa uharibifu wowote wanaofanya kwa vifaa au programu za kompyuta.
- Uchapaji unapatikana katika kompyuta za umma. Maktaba Wanachama zitaweka bei na njia za uchapaji na huduma nyingine za kompyuta. Gharama hizi zinaweza kutofautiana kati ya eneo na eneo.

## MAJIBU KUHUSU UKIUKAJI

Ufikio wa mtumiaji kwa muunganisho wa kompyuta wa maktaba na Intaneti ni upendeleo, si haki. Mtumiaji anakiuka sera hii kupitia hatua binafsi ya mtumiaji. Kushindwa kutii sera hii na taratibu zake itasababisha kunyang'anywa ufikio wa mtumiaji wa kompyuta katika **Maktaba Wanachama zozote za Mfumo wa Maktaba wa Kaunti ya Lancaster**. Kosa la kwanza litasababisha kupoteza haki ya kompyuta kwa mwezi mmoja. Kosa la kwanza litasababisha kupoteza haki ya kompyuta kwa miezi sita. Baada ya kosa la tatu, mtumiaji atapoteza haki zote za kompyuta kwa muda usiojulikana. Uamuzi kuhusu jibu linalofaa kuhusu ukiukaji utatolewa na Mkurugenzi wa Maktaba Mwanachama ambapo kosa lilifanyika, au na mteule wake. Rufani ziwe kwa maandishi na ziwasilishwe kwa Mkurugenzi wa Maktaba Mwanachama. Majibu yatatolewa ndani ya siku 30 baada ya kupokea rufani. Ufikio wa maktaba za umma za Kaunti unaweza kusitishwa hadi Mkurugenzi atoe jibu la maandishi kwa rufani hiyo.

## HAKIMILIKI

Sheria ya hakimiliki ya Marekani (Title 17, U.S. Code) inakataza urudufishaji au usambazaji usio na idhini wa nyenzo zenye hakimiliki isipokuwa imeruhusiwa na kanuni za "matumizi ya haki". Watumiaji hawapaswi kunakili au kusambaza nyenzo za kielektroniki (ikiwemo maandishi, picha, programu, barua pepe au data) bila idhini ya wazi ya mwenye hakimiliki. Wajibu wa matokeo ya ukiukaji wa hakimiliki ni wa mtumiaji pekee, kwani Maktaba Wanachama wa LSLC wanakanusha waziwazi dhamana au wajibu wowote unaotokana na matumizi hayo.